**KISWAHILI**
**KIDATO CHA KWANZA**
**MTIHANI WA KUFUNGUA MUHULA WA 2 - 2024**

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

## SEHEMU YA A. INSHA

Mwandikie mwalimu mkuu wa shule yako ya Upili barua ukimweleza mambo ambayo yafaa kuzingatiwa ili kumarisha masomo shuleni. (alama 20)

## SEHEMU YA B. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.

### NDOTO YANGU

Kila mara huwa ninawaza na kuwazua juu ya maisha yangu ya usoni. Fikra zangu hupaa mithili ya chombo cha angani kutafuta jawabu la kutegua kitendawili cha maisha yangu ya baadaye.

Azma niliyonayo maishani ni ndoto. Ni ndoto ya muda mrefu mfano wa kiu inayosumbua nafsi yangu. Ndoto hiyo ni ile ya kuwa mkulima.

Zaraa ni kazi yenye mvuto mkubwa kwangu. Nimwonapo mkulima amejipinda, jembe mkononi, mgongo kauachilia jua limchome litakavyo, misuli imemtutumika na macho kayakaza kwa ari, moyo wangu huchanuka kwa furaha mfano wa ua la alfajiri. Furaha yangu ni nimwone mkulima mwenye himaya ya shamba kubwa lenye mashine na matrekta huku wafanyakazi wakijizatiti kulihudumia.

Ninasahabu kuwa mkulima kwani tajiri wangu atakuwa Maulana katika kuajiriwa na mwanadamu mwenzangu. Mkulima anapotayarisha shamba lake huwa anaweka matumaini yake kwa Rabuka. Kuchipuka na kuota kwa mbegu alizozifukia hutegemea mapenzi yaMuumba wake. Vilevile, mifugo wake huongezeka kutokana na Baraka za Mola, kinyume cha kazi ambayo ujira unatokana na kupipwa na tahuru – binadamu.

Furaha yangu kama mkulima ni kusimama juu ya kichuguu ili nishibishe macho yangu kwa mandhari yenye kuvutia. Mandhari ya ardhi yenye miti na mimea iliyofunika na kutanda kama vile zulia za la kijani. Nione pia mifugo wengi wakijilia majani na nyasi bila hofu. Sauti zao zikisikika zikipokesana kana kwamba wanatoa shukrani kwa Muumba wao.

Nitaridhika nionapo vijulanga wenye afya kutokana na lishe bora wakicheza na kurukaruka. Watoto wenye nyuso zinazobashiri matumaini maishani. Vile vile, ni furaha iliyoje kuona wananchi wanaopata lishe bora ya kuwapa nguvu na afya kwa minajili ya kujenga taifa lao!

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Kama mkulima nitachukua jukumu la kuwahamasisha wananchi kutilia maanani umuhimu wa kuhifadhi udongo na kutunza vyanzo vya maji kwa kutokokata miti kiholela.

Natarajia kuwa mkulima ili nijiunge na wakulima wenzangu nchini. Kwa lengo la kuikinga jamii yetu dhidi ya njaa. Nchi isiyo na chakula cha kutosha cha kuwalisha raia wake huwa na matatizo. Tatizo mojawapo ni kulazimika kuagiza chakula kutoka nchi zingine. Hii huleta hali ya utegemezi na matumizi ya juu ya fedha za nchi.

Ndoto yangu ni kuona watu wakipata ajira kutokana na kilimo. Waama ajira mashambani au katika viwanda huhitaji malighafi kutoka kwenye sekta ya zaraa. Nitaridhika mno nionapo wafanyakazi nitakaowaajiri wakiimarisha maisha yao.

Wanafunzi wenzangu hushangaa kuona vile ninavyuopenda zaraa. Wao hawajui nia yangu. Nia hiyo ni ile ya kuitimiza ndoto yangu kwani safari ya kesho hufungwa leo.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

**<u>MASWALI:</u>**

1. Eleza sababu za mwandishi katika kuwa mkulima. (alama 2)
   - **Mwajiri wake atakuwa Mwenyezi Mungu wala si binadamu. Anapopanda mbegu ni Mwenyezi Mungu ndiye husababisha ziote.**
   - **Atakuwa na mifugo ambao watanawirishwa na Mwenyezi Mungu.**
   - **Kutazama miti na mimea iliyoota barabarani kungempendeza.**
   - **Kufurahia mifugo wengi wakila nyasi na majani.**
   - **Kutazama kwa furaha watoto wenyeafyawakicheza na kurukaruka kwa sababu ya lishe bora.**
   - **Kuwaona wananchi wapatao lishe bora ya kuwapa nguvu na afya ili kujenga taifa.**

2. Ni vipi tajiri wa mkulima ni maulana? (alama 2
   - **Tajiri wa mkulima ni Maulana kwa sababu ndiyemwenye uwezo wa kuchipuza na kuotesha mbegu zilizopandwa. Mkulima, yake ni kutia matumaini tu.**
   - **Mwenyesi Mungu ndiye ataneemesha mifugo ili wanawiri.**

3. Umuhimu wa lishe bora ni upi? (alama 1)

   Humsaidia mtu kuwa na afya bora inayomwezesha kufanyakazi.

4. Taja aina za kilimo zilizoelezwa katika habari. (alama 2)
   - **Kilimo cha mimea**
   - **Kilimo cha ufugaji**

5. Eleza maana ya Maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 3)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(a) Azma – **Maono, ari.**

(b) Ninastahabu – **Ninafurahia, ninapenda**

(c) Kiholela – **Ovyo, bila mpangilio**

## SEHEMU YA C. MATUMIZI YA LUGHA: ALAMA 30

1. Huku ukitolea mifano, eleza aina mbili kuu za ala za matamshi. (alama 4)
    - **Ala tuli – Ala ambazo huzisogei sauti inapotamkwa. Mfano: ufizi, meno.**
    - **Ala sogezi – Ala ambazo hazisogea sauti inapotamkwa. Mfano: midomo, ulimi.**

2. Taja sifa za sauti zifuatazo:- (alama 2)
    **/b/ - hutamkiwa midomoni. (alama ½ )**
    **//w/ - sauti ghuna (alama ½ )**
    **- Kiyeyusho/Nusu irabu (alama ½ )**

3. Ukizingatia kigezo cha jinsi hewa inavyozuiliwa, taja aina zozote mbili za Konsonanti. (alama 2)
    - **Kimadende**
    - **Kitambaza**
    - **Nazali n.k.**

4. Taja maneno mawili yenye sauti mwambatano ya midomoni. (alama 2)

    **Bweni, umbo, pweza**

5. Weka Shadda kwenye Maneno haya yalete maana iliyo mabanoni. (alama 2

    Ala – (Kifaa/Chombo) – **'Ala**

    Walakini – (Dosari/Kasoro) – **Wa'lakini**

6. Taja aina mbili za viambishi. (alama 2)
    **(i) Viambishi awali**
    **(ii) Viambishi vikuu**

7. Ukianza na cha chini zaidi, taja vipasho vya lugha. (alama 2)

    Sauti ⟶ Silabi ⟶ Neno ⟶ Sentensi

8. Onyesha aina za maneno katika sentensi ifuatazo. (alama 2 ½)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Alienda mjini kwa minajili ya kutafuta kazi.
**T E U T N**

9. Tambulisha na ufafanue viambishi vilivyotumika katika neno hili:-
Apikavyo (alama 2)
A – Nafsi/Ngeli
Pik – mzizi
a - Kauli/kiishio
vyo - kirejeshi

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

10. Taja matumizi mawili ya alama ya Koloni. (alama 2)
(i) Kutenga saa na dakika

(ii) Kuonyesha kuna orodha inayofuata.

11. Andika sentensi zifuatazo katika wingi. (alama 1)
(i) Ulezi wa kumwendekeza mtoto haufai.
Malezi ya kuwaendekeza watoto hayafai

(ii) Maarifa aliyoyatafuta hayakumfaa.
Maarifa waliyoyatafuta hayakuwafaa

Teacher.co.ke

12. Majina yafuatayo yamo katika Ngeli gani? (alama 2)
Ulezi – **U - YA**

Maji – **YA - YA**

Kitabu – **KI - VI**

Sokwe – **A - WA**

13. Kamilisha methali zifuatazo:- (alama 2)

(i) Chema chajiuza ……**kibaya chajitembeza**……..

(ii) Ukiona vyaelea ……**jua vimeundwa**……

14. Sahihisha sentensizi zifuatazo. (alama 1)
(i) Mashamba zimelimwa vizuri
**Mashamba yamelimwa vizuri**
(ii) Jicho yake itapona.
**Jicho lake litapona**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

15. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kiambishi sahihi. (alama 1)

(i) Chombo kipya ___**Ki**__menunuliwa

(ii) Vyeo walivyopewa _**Vi**__mewafurishwa vichwa.

16. Tumia maneno yaliyo mabanoni kukamilisha sentensi zifuatazo. (alama 2)

(yumo, kule, mlimo, kuna, kwenye, popote, ndipo)

(i) Nyoka ______ **yumo** . pangoni.

(ii) ____ **Kwenye** _ miti hakuna wajenzi.

17. Andika maneno mawili yenye muundo ufuatao. (alama 1)

K + I + K + I - **Kuwa** (alama ½ )

I + I - **au** (alama ½ )

**SEHEMU YA D: ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

Mchuuzi 1: Karibu Kastoma nikuuzie. Hujambo?
Mchuuzi 2: Sijambo mama
Mchuuzi 1: Nikuuzie nini? Chagua nitakupimia vizuri.

(a) Tambua sajili hii. (alama 2)

**Sokoni/Biashara**

(b) Taja sifa zozote nane za sajili uliyoitaja. (alama 8)

**(i) Msamiati maalum wa kibiashara kama vile pesa, bei, mnunuzi n.k.**
**(ii) Lugha huwa changamfu na ya kupendeza.**
**(iii) Lugha huwa ya kushawishi wanunuzi.**
**(iv) Utohozi hutumiwa kama vile Kastoma.**
**(v) Kuna kuchanganya ndimi.**
**(vi) Kuna matumizi ya lugha ya kushawishi.**
**(vii) Wakati mwingine lugha yake si sahihi.**
**(viii) Lugha huweza kuambatanishwa na viziada lugha.**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes